


# ATTENTION! HATARI!



Ngozi nyeusi inailinda ngozi yako na miale ya jua. Lakini mafuta yanayosababisha ngozi yako kuwa nyeupe, inaharibu ngozi na afya yako. Mafuta haya yana vitu vifuatavyo ndani yake:

## Hydroquinone

- Inasababisha ngozi yako kuwa na madoa meusi (“ochronosis”)
- Matokeo yake ni kuwa na “patches” kwenye ngozi yako na pia ngozi inaharibika
- Mafuta hayo yakiingia machoni yanaweza kusababisha upovu
- Wanyama waliopakwa mafuta hayo walipata kansa ya damu, uvumbi wa ini na wengu

## Corticosteroids

(hydrocortisone, betametasone etc.)

- Inachelewesha uponaji wa vidonda
- Inaathiri akili na macho
- Inapunguza kinga ya mwili
- Inasababisha ukuaji wa nywele usoni
- Ngozi inaanza kuwa nyepesi kama “karatasi” – na kufanana kama ngozi ya ki-uzee
- Inaweza kusababisha kisukari, shida za mifupa na upungufu wa nguvu za kiume

## Mercury (Zebaki)

- Ni kemikali hatari sana. Sumu yake inaharibu mwili kwa kudumu
- Inafanya ngozi kuwa kavu sana na kuwa na mabakamabaka, upele nk
- Inasababisha madoa mweusi kwenye ngozi
- Mercury inaathiri akili na kusababisha kupoteza kumbukumbu
- Mercury inaathiri akili ya mtoto aliye tumboni mwa mama yake
- Inaathiri viungo vya uzazi na kusababisha kutokuzaa
- Mercury inaathiri mazingira kwa milioni ya miaka
- Ulaya uuzaji wa Mercury ulipigwa marufuku na mtu akiuza, inamfikisha gerezani!!

“Hamjui kwamba miili yenu ni Hekalu la Roho Mtakatifu”? 1 Cor. 6:19

[www.anamed.net](http://www.anamed.net)  
anamed poster nr. 453 (Swahili)

Bango hili limechorwa na kuchapwa na Waafrica kwa Waafrica kwa ajili ya kampeni ya “Nyeusi ni mzuri”. Uionge mkono kampeni hiyo na mgawe bango hilo!! Kampeni hii imeungwa mkono na: vikundi vya anamed America Kusini na Ulaya ([www.anamed.net](http://www.anamed.net)), AICT HUYAMU Tanzania ([www.huyamu.info](http://www.huyamu.info)), European Herbal and Traditional Medicine Association ([www.ehtpa.eu](http://www.ehtpa.eu)), GIFTS in UK ([www.giftsofhealth.org](http://www.giftsofhealth.org)), International Foundation of Dermatology in UK ([www.ifd.org](http://www.ifd.org)), Phoenix Integrated Health in UK and Malawi ([www.phoenixclinic.org.uk](http://www.phoenixclinic.org.uk)), REAP in Kenya ([www.reap-eastafrika.org](http://www.reap-eastafrika.org)), GEUS in Denmark ([www.geus.dk](http://www.geus.dk)). Picha: anamed Kinshasa ([anamed\\_kin@yahoo.fr](mailto:anamed_kin@yahoo.fr)), Maneno: anamed Cameroon ([anamedbda2008@yahoo.com](mailto:anamedbda2008@yahoo.com)). **Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO)** limetaka ichukuliwe hatua ya kupiga marufuku utengenezaji na utumiaji wa vipodozi vyenye kemikali ya mercury. Himiza Kikundi cha anamed kilicho kwenye nchi yako kutengeneza vipodozi visivo na madhara kwako.